SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UVUVI, NAM. 7 YA 2010 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA MAENDELEO YA UVUVI NA UHIFADHI WA BAHARI KWA AJILI YA KUSIMAMIA, KUENDELEZA UVUVI NA KUHIFADHI MALIASILI ZA BAHARINI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

MPANGILIO WA VIFUNGU

VIFUNGU **MAELEZO**

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI WA MAMLAKA

4. Uanzishwaji wa Mamlaka.
5. Muhuri na nembo ya Mamlaka
6. Kazi za Mamlaka.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

7. Uanzishwaji na muundo wa Bodi.
8. Sifa za Mwenyekiti.
9. Katibu wa Bodi.
10. Kazi za Bodi.
11. Uwezo wa Bodi.
12. Mwenendo wa Bodi.
13. Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.



14. Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

15 Idara, vitego na divisheni.

16. Wafanyakazi wa Mamlaka.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI WA UVUVI

17. Mipango ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi.

18. Hatua za usimamizi wa uvuvi.

19. Uteuzi wa Maafisa walioidhinishwa.

20. Wakaguzi wa Uvuvi.

21. Waangalizi wa uvuvi.

22. Uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa mitego ya uvuvi na vifaa.

23. Katazo la mitego, vifaa na mbinu za uvuvi haribifu.

24. Katazo la uvuvi, ushushaji na uuzaji wa samaki.

25. Uwekaji wa vifaa vya kuvutia samaki au mwamba bandia.

26. Katazo la kuvuruga au kuharibu mtego wa uvuvi.

27. Ufuatiliaji.

28. Ushajishaji wa uvuvi mdogo na kusaidia uvuvi wa viwanda.

29. Kutangazwa kwa diko na bandari ya uvuvi.

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA WAVUVI NA UTOAJI LESENI WA VYOMBO VYA UVUVI

30. Usajili wa shughuli za uvuvi.

31. Leseni za uvuvi.

32. Usimamishaji au Ufutaji wa leseni.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI WA UKUZAJI WA VIUMBE MAJI

33. Usajili wa miundombinu na shughuli za ukuzaji wa viumbe maji.

34. Uendeshaji wa shughuli za ukuzaji wa viumbe maji

35. Uingizaji, uhamishaji na usafirishaji nje wa viumbe vya maji ya baharini na maji baridi na bidhaa zake.

36. Vibali vya ukuzaji wa viumbe maji.

37. Ujenzi, uendeshaji na uondoaji wa miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji.

38. Udhibiti wa maradhi.

39. Hatua za kuzuia.

SEHEMU YA SABA
USIMAMIZI NA VIWANGO VYA UBORA VYA SAMAKI NA BIDHAA ZA MAJINI

40. Mamlaka yenye uwezo.

41. Uingizaji wa samaki hai.

42. Taratibu za karantini kwa ajili ya uingizaji wa samaki hai wa mapambo.

43. Katazo la kutupa au kuachia samaki hai wa mapambo aliyeingizwa.

SEHEMU YA NANE
UHIFADHI WA USIMAMIZI WA BAHARI

44. Kutangazwa Maeneo ya uhifadhi wa bahari.

45. Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari.

46. Hatua za usimamizi wa uhifadhi.

47. Ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya bahari.

48. Uanzishwaji wa ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini kwenye kizuizi maalum.

49. Ulinzi wa viumbe vilivyo hatarini kutoweka au vilivyohifadhiwa.

50. Utangazaji na uhifadhi wa viumbe adimu, waliyopo kwenye tishio au waliyo hatarini kutoweka.



51. Katazo la kuwinda, kuua na kujeruhi mamalia wa baharini na viumbe vyote vya jamii ya kasa.

52. Ulinzi wa eneo maalumu na eneo la kurejesha rasilimali za uvuvi.

53. Uchafuzi wa maeneo ya bahari.

54. Masharti ya kibali katika eneo la bahari.

55. Mkakati wa ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA FEDHA

56. Fedha na rasilimali za Mamlaka.

57. Bajeti ya Mamlaka.

58. Hesabu na ukaguzi.

59. Ufunguaji wa hesabu za benki

SEHEMU YA KUMI
MAKOSA NA ADHABU

60. Makosa na Adhabu.

61. Adhabu ya Ziada.

62. Adhabu ya Jumla.

63. Kumaliza kosa.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MASHARTI MENGINEYO

64. Uanzishwaji wa Kamati za Usimamizi wa pamoja.

65. Daftari la kumbuklumbu.

66. Vitu vyenye asili ya kuharibika.

67. Rufaa.

68. Kanuni.

69. Kufuta na kubakiza.

JADWELI

SHERIA NAM. 4 YA 2026

NIMESAINI

{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

.....19/10/....., 2026

SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UVUVI, NAM. 7 YA 2010 NA KUTUNGA SHERIA YA MAMLAKA YA MAENDELEO YA UVUVI NA UHIFADHI WA BAHARI KWA AJILI YA KUSIMAMIA, KUENDELEZA UVUVI NA KUHIFADHI MALIASILI ZA BAHARINI NA KUWEKA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

IMETUNGWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari, 2026 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

2. Sheria hii itatumika kwa masuala yote yanayohusiana na usimamizi na uendelezaji wa uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na uhifadhi wa bahari Zanzibar.

Ufafanuzi.

3. Katika Sheria hii, isipokuwa maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Bandari ya uvuvi" maana yake ni Bandari ya uvuvi yenye kutoa huduma za kushushia, kupakia, kusarifu, kuhifadhi na kuuza samaki;

"bidhaa za mimea au wanyama wa maji ya baharini na maji baridi" maana yake ni kitu chochote kilichotengenezwa na, au kimeundwa na mimea au wanyama wa maji ya baharini na maji baridi au sehemu yake;

"bidhaa ya samaki" maana yake ni bidhaa inayopatikana kwa usindikaji wa samaki inayokusudiwa kutumika kama chakula cha binadamu na wanyama au malighafi katika kutengeneza bidhaa nyengine za kibiashara au mapambo;

"bioanuwai" maana yake ni utofauti miongoni mwa viumbe hai kutoka katika vyanzo vyote, ikijumuisha mazingira ya ardhini, baharini na ikolojia ya viumbe wengine na mchanganyiko baina yao kwenye ikolojia;

"chombo cha uvuvi" maana yake ni boti au chombo cha baharini kinachotumika au kinachotegenezwa kwa ajili ya kuvulia, kuchakata au kusafirisha samaki au mazao ya samaki;

"Diko" maana yake ni eneo la kushushia samaki kwa hatua ya awali, mazao ya samaki au mazao ya mimea ya baharini na kutoa sehemu ambayo wavuvi wanaweza kuacha boti zao na kupata huduma mbali mbali kama vile chakula, mafuta na barafu;

"jicho" maana yake ni uwazi au nafasi katika nyavu au dema iliyozungukwa na uzi, waya au mti iliyochongwa;

"juya" maana yake ni aina ya uvuvi ambao hutumia nyavu kuvulia au zana za kuvulia za kuzungushia inayojumuisha kipande au vipande vya nyavu chini ya inchi mbili vilivyowekwa kati ya kamba mbili, na vinaweza kuambatanishwa na vifaa vya kuzungushia vilivyotengenezwa kwa kipande au vipande vya nyavu zenye upana wa chini ya inchi mbili majani ya miti, matawi, nguo, mifuko, au majani ya mitende, ambayo njia yake ya kufanya kazi inahusisha uvutaji wa nyavu au zana hiyo kuelekea ufukweni, mafungu ya mchanga, eneo la maji ya kina kifupi, au juu ya chombo cha uvuvi kwa kuvuta kamba;

"Maeneo ya Uhifadhi wa Bahari" maana yake ni eneo lolote lililotangazwa kuwa Eneo la Uhifadhi wa Bahari chini ya kifungu cha 44(1) cha Sheria hii;

"maji ya Nchi" maana yake ni maji ya ndani ya eneo linaloongezeka baharini katika masafa ya maili kumi na mbili kutoka katika mstari wa asili wa mwambao wa kina kidogo wa Zanzibar;

"maji ya ndani" maana yake ni eneo lolote la baharini ambalo lipo upande wa ardhini kutoka katika mstari wa asili unaoyagawa maji ya baharini ya kitaifa na maji ya bahari ya eneo la bahari ya Zanzibar;

"maliasili za bahari" maana yake ni maliasili zinazopatikana ndani ya bahari;



"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari iliyoanzishwa chini ya masharti ya kifungu cha 4(1) cha Sheria hii;

"mfumo wa ikolojia ya bahari" maana yake ni mkusanyiko wa viumbe hai katika mazingira ya bahari;

"mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi" maana yake ni aina zote za jamii ya mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi;

"miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji" inajumuisha vizimba vya samaki, mitego ya samaki, vituo vya kutotolea vifaranga vya samaki, maeneo ya kufugia samaki, mabwawa ya samaki, mashamba ya mwani, mashamba ya majongoo wa baharini na miundombinu mengine yote inayohusiana na shughuli za ufugaji wa viumbe wa majini;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 13(1) cha Sheria hii;

"Mvuvi" maana yake ni mtu ambaye anajihusisha na shughuli za uvuvi kwa madhumuni ya kujipatia chakula au kufanya biashara kwa kuvua samaki au rasilimali nyengine za bahari;

"nyavu ya kuvulia" maana yake ni zana iliyotengenezwa kwa uzi au malighafi nyengine inayotumika kuwazingira, kuwashika au kuwatega samaki ambayo inafungwa kwa kamba ili kuweka macho yake wazi;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"samaki aliyeharibiwa" maana yake samaki aliyevuliwa kwa kutumia mripuko, sumu au chemikali nyengine ambazo zinaweza kusababisha sumu katika chakula;

"shughuli ya uvuvi" maana yake ni shughuli yoyote inayohusisha uvunaji wa samaki ikijumuisha ukamataji au ukuzaji wa viumbe maji, utafutaji wa samaki, uchakataji, urekebishaji wa vyombo vya uvuvi, usafirishaji sokoni na shughuli nyengine zozote ambazo zinahusika katika mnyororo wa thamani;

"uhifadhi" maana yake uangalizi na ulinzi wa maliasili za baharini na pwani ili ziweze kutoa huduma kwa kizazi cha sasa na cha baadae;

"uendelezaji" maana yake ni kitendo au mchakato wa kuendeleza, kukuza, au kuimarisha uvuvi, mradi, au rasilimali ili ifikie hatua ya juu zaidi au izidi kuzalisha matunda;

"ukuzaji wa viumbe maji" maana yake ni ukulima au kitendo cha kuzalisha, kukuza na kuvuna mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi katika mazingira ya maji ya baharini au maji baridi;

"uvuvi" maana yake ni kuvua samaki au viumbe maji wengine kutoka katika maeneo yao ya makaazi;

"uvuvi wa kiwanda" maana yake ni uvuvi unaojumuisha vyombo vya baharini juu ya mita ishirini na nne;

"uvuvi mdogo" maana yake ni uvuvi unaotumia vyombo vya baharini juu ya mita kumi na mbili na chini ya mita ishirini na nne;

"viumbe adimu waliyopo kwenye tishio au waliyo hatarini kutoweka" maana yake ni mimea au wanyama wa maji ya baharini na maji baridi ikijumuisha aina tofauti za matumbawe na makome ambayo yapo hatarini kutoweka kama ilivyoelezwa katika sheria za uvuvi na Mkataba wa Kibiashara wa Kimataifa ya Aina za Mimea na Wanyama Waliohatarini Kutoweka;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na uvuvi na uhifadhi wa bahari; na

"wavuvi wadogo wadogo" maana yake ni wavuvi ikijumuisha wavuvi wa mguu na vyombo ambavyo vipo chini ya mita kumi na mbili.

SEHEMU YA PILI
UANZISHWAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji wa Mamlaka.

4.-(1) Kunaanzishwa Mamlaka itakayojulikana kama Mamlaka ya Maendeleo ya Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari.

(2) Mamlaka itakuwa ni chombo kinachojitegemea, chenye urithi wa kuendelea, chenye muhuri wake na kwa jina lake, kwa mujibu wa sheria, kitakuwa na uwezo wa:

(a) kushtaki na kushtakiwa;

(b) kupata, kumiliki, kununua au kuondosha mali yoyote inayohamishika au isiyohamishika;

(c) kuingia katika mkataba au muamala wowote;

(d) kukopa au kukopesha kiwango chochote cha fedha; na

(e) kutekeleza au kufanya kitendo au jambo lolote ambalo chombo kinachojitegemea kinaweza kulitekeleza au kufanya.

Muhuri na nembo ya Mamlaka.

5.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoweza kuamuliwa na Bodi.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Mamlaka katika waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Mkurugenzi Mkuu au afisa mwengine yeyote wa Mamlaka aliyeidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(3) Waraka wowote utakaokusudiwa kuwa ni hati inayotolewa na Mamlaka utawekwa muhuri wa Mamlaka na utathibitishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Kazi za Mamlaka.

6.-(1) Mamlaka itakuwa na majukumu ya kukuza uvuvi endelevu, ukuzaji wa viumbe maji na uhifadhi wa bahari.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka itakuwa na kazi za:

(a) kusimamia na kuendeleza uvuvi endelevu na shughuli za ukuzaji wa viumbe maji;

(b) kusajili miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji;

(c) kudhibiti, kuhifadhi na kusimamia maeneo ya hifadhi za bahari, maeneo maalumu na maeneo ya kurejesha rasilimali za uvuvi na bioanuai za fukwe na za baharini;

(d) kudhibiti na kushajihisha matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji, udhibiti wa ubora na uongezaji wa thamani;

(e) kutoa leseni na kibali kwa ajili ya shughuli za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji, na shughuli zinazofanywa ndani ya maeneo ya uhifadhi wa bahari;

(f) kukuza na kusimamia masoko ya samaki na usambazaji wa bidhaa za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji katika mnyororo wa thamani;

(g) kuratibu uhifadhi sahihi na matumizi endelevu ya fukwe na maliasili za bahari;

(h) kutoa miongozo ya usimamizi bora ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na uhifadhi wa bahari;

(i) kupendekeza maeneo ya utafiti kwa taasisi husika yanayohusiana na uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji na uhifadhi wa bahari;

(j) kushirikiana na taasisi nyengine za kitaifa, kikanda na kimataifa au jamii juu ya usimamizi wa uvuvi na ukuzaji viumbe maji na uhifadhi wa fukwe na bahari;

(k) kukuza na kuhifadhi shughuli za asili za usimamizi wa uvuvi; na

(l) kufanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoonekana inafaa katika kutimiza malengo ya Sheria hii.

SEHEMU YA TATU
USIMAMIZI NA UENDESHAJI WA MAMLAKA

Uanzishwaji na muundo wa Bodi.

7.-(1) Kutakuwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ambayo itaundwa na:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Mkuu;

(c) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(d) mwakilishi mmoja kutoka:

(i) Wizara inayohusika na uvuvi na uhifadhi wa bahari;

(ii) Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar;

(iii) Taasisi au jumuiya kutoka sekta binafsi inayohusiana na uvuvi au uhifadhi wa Bahari; na

(iv) Jumuiya za Wavuvi.

(2) Wajumbe chini ya kifungu kidogo cha (1)(c) na (d) cha kifungu hiki watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na wakuu wa taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, taaluma na jinsia zao.

Sifa za Mwenyekiti.

8. Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba na uweledi wa hali ya juu wa kusimamia masuala ya taasisi za umma au binafsi kwa ufanisi; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Katibu wa Bodi.

9.-(1) Bodi itamteua mfanyakazi wa Mamlaka kuwa Katibu wa Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Katibu wa Bodi ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria au mwenye sifa ya kuwa katibu wa shirika kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali; na

(b) uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi, na:

(a) kwa kushauriana na Mwenyekiti ataandaa ajenda za vikao vya Bodi;

(b) atachukua kumbukumbu sahihi za vikao vya Bodi;

(c) atatunza kumbukumbu sahihi na zenye kujitosheleza za Bodi;

(d) atatoa taarifa sahihi za vikao vya Bodi kwa wajumbe; na

(e) atafanya kazi nyengine yoyote kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Kazi za Bodi.

10. Kazi za Bodi zitakuwa ni:

(a) kutoa miongozo ya kimkakati kwa Mamlaka;

(b) kusimamia uendeshaji na utekelezaji wa jumla wa Mamlaka;

(c) kupitia na kuidhinisha miongozo, mipango, malengo na shabaha za kazi sahihi za Mamlaka;

(d) kuamua mikakati au sera zinazosimamia uendeshaji wa Mamlaka; na

(e) kutekeleza kazi nyengine zozote kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hii.

Uwezo wa Bodi.

11. Uwezo wa Bodi utakuwa ni:

(a) kumuelekeza Mkurugenzi Mkuu kuipatia Bodi taaarifa, ripoti au nyaraka nyengine ambayo Bodi itaona ni muhimu;

(b) kutoa maelekezo halali kwa Mkurugenzi Mkuu kuhusiana na usimamizi na utekelezaji wa Mamlaka;

(c) kuandaa Kanuni za Fedha na Kanuni za Utumishi;

(d) kuidhinisha bajeti ya Mamlaka;

(e) kuidhinisha ada na tozo;

(f) kupendekeza muundo wa utumishi wa Mamlaka;

(g) kuajiri wafanyakazi wa Mamlaka kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011; na

(h) kutoa miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

Mwenendo wa Bodi.

12. Masharti yanayohusiana na mwenendo wa Bodi yatakuwa kama yalivyoainishwa katika Jadweli la Sheria hii.

Uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

13.-(1) Kutakuwa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ambaye atateuliwa na Rais.

(2) Mtu atakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu ikiwa mtu huyo ana:

(a) angalau shahada ya kwanza katika fani ya uvuvi, ukuzaji wa viumbe maji, sayansi ya bahari, sayansi ya mazingira au fani nyengine yoyote inayolingana kutoka katika taasisi inayotambuliwa na Serikali;

(b) uzoefu wa kazi wa angalau miaka saba; na

(c) uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mkurugenzi Mkuu.

14.-(1) Mkurugenzi Mkuu atakuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka na atawajibika kwa kazi, utekelezaji na usimamizi wa kila siku wa Mamlaka.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu:

(a) atasimamia utekelezaji wa malengo, sera na kanuni za Mamlaka na kutoa taarifa kwa Bodi;

(b) atasimamia fedha na samani za Mamlaka kwa mujibu wa sheria husika;

(c) atasimamia na kudhibiti nidhamu za wafanyakazi wa Mamlaka; na

(d) atatekeleza kazi nyengine yoyote muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa sheria hii kama atakavyoelekezwa na Bodi.

Idara, vitengo na divisheni.

15.-(1) Mamlaka itaanzisha idara, vitengo au divisheni kama itakavyoona inafaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

(2) Wakuu wa idara na vitengo watateuliwa na Bodi kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(3) Wakuu wa divisheni watateuliwa na Mkurugenzi Mkuu kwa kuzingatia sifa na uzoefu wao.

(4) Wakuu wa idara, vitengo na divisheni watawajibika kwa Mkurugenzi Mkuu.

Wafanyakazi wa Mamlaka.

16. Mamlaka inaweza kuajiri wafanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

SEHEMU YA NNE
USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA UVUVI

Mipango ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi.

17.-(1) Mamlaka itaandaa na kufanya mapitio ya mipango ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi.

(2) Mipango itaainisha hali ya uvuvi, malengo yanayokusudiwa kufikiwa na hatua za usimamizi, uendelezaji na utoaji wa leseni zitakazotumika, ikijumuisha kiwango cha uvuvi, ambacho kitawekwa katika chombo cha uvuvi.

(3) Mamlaka, katika kuandaa mpango wa usimamizi na uendelezaji wa kila uvuvi, itashauriana na wavuvi wa ndani na watu wengine watakaoathirika na mpango huo.

(4) Mamlaka, pale inapohitajika, itashauriana na mamlaka za usimamizi wa uvuvi na hususan zile zinazotumia maeneo ya pamoja ya uvuvi au samaki wanaohama kwa lengo la kuhakikisha usawa katika mipango yao husika ya usimamizi na uendelezaji wa uvuvi.

(5) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "mamlaka za usimamizi wa uvuvi" maana yake ni mamlaka au taasisi za uvuvi nyengine zinazohusika na usimamizi wa uvuvi nje ya Zanzibar.

Hatua za usimamizi wa uvuvi.

18. Mkurugenzi Mkuu kwa kushauriana na wavuvi anaweza kuweka hatua yoyote kati ya zifuatazo kwa ajili ya usimamizi bora wa uvuvi:

(a) kudhibiti njia za uvuvi na zana ikijumuisha ukubwa wa jicho la nyavu au dema ambalo litatumika kwa ajili ya uvuvi;

(b) kudhibiti kiwango, ukubwa na sifa nyengine za samaki ambao wanaweza kuvuliwa, kushushwa au kuuzwa;

(c) kutangaza ufungaji wa muda wa eneo lililotengwa kwa ajili ya aina ya samaki, mitego au njia ya uvuvi;

(d) kupendekeza kwa Waziri maeneo sahihi kwa ajili ya uhifadhi na kiwango cha kuvua samaki; na

(e) kuzuia uharibifu na uchafuzi wa maeneo ya uvuvi.

Uteuzi wa Maafisa walioidhinishwa.

19.-(1) Mkurugenzi Mkuu atateua afisa kutoka ndani au nje ya Mamlaka kuwa afisa aliyeidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza Sheria hii.

(2) Uteuzi wa maafisa walioidhinishwa kutoka nje ya Mamlaka utafanywa kwa kushauriana na taasisi husika.

(3) Afisa aliyeidhinishwa na kuteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki anaweza, wakati wowote na kwa msaada wa kisheria, kwa kibali au bila kibali:

(a) kuingia na kupekua ndani ya jengo, chombo cha moto, ndege, chombo cha baharini au sehemu nyengine yoyote inayoshukiwa;

(b) kuchukua, kuzuia, kuondoa au kuhifadhi taarifa na ushahidi;

(c) kukamata mali yoyote ambayo imeonekana ikihusika na ukiukwaji wa masharti yoyote ya Sheria hii;

(d) kumkamata mtu yeyote anayeshukiwa kufanya kosa chini ya Sheria hii;

(e) kuchukua sampuli kwa ajili ya kupima na ushahidi;

(f) kutaka ushahidi wa nyaraka;

(g) kuondoa sehemu yoyote kutoka katika chombo cha moto, ndege, chombo cha baharini au miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji iliyokamatwa;

(h) kutaka taarifa kutoka kwa mtu yeyote mwenye maslahi;

(i) kuamuru kuondolewa kwa uchafu wowote, taka, au kitu chengine chochote kilichothibitishwa kuwa na madhara kwa mazingira ya maji ya baharini na maji baridi; na

(j) kufuatilia lalamiko lolote lililowasilishwa kwa Mamlaka na kuchukua hatua.

Wakaguzi wa Uvuvi.

20.-(1) Mkurugenzi Mkuu, kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti Rasmi, atateua maafisa wenye sifa miongoni mwa maafisa waliyoidhinishwa kuwa wakaguzi wa uvuvi.

(2) Wakaguzi wa uvuvi walioteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki wanaweza, wakati wowote, na kwa msaada wa kisheria na bila ya kibali:

(a) kusimamisha, kuingia na kukagua chombo chochote cha baharini, mitego yake, rasilimali za uvuvi, shehena, kifaa, ghala, hati au kitu chengine chochote kinachohitajika kuwekwa chini Sheria hii;

(b) kuingia na kukagua jengo au chombo cha moto ambacho anashuku kuwa rasilimali za uvuvi au vifaa vya uvuvi vinahifadhiwa au kusafirishwa;

(c) kuchunguza mtego wa uvuvi wowote au kifaa ambacho kimetumika au kinachokusudiwa kutumika katika kuvuna, kutunza au kuchakata rasilimali za uvuvi;

(d) kumhoji mtu yeyote ambaye, kwa maoni yake, anaweza kutoa taarifa zozote ambazo anaweza kuzihitaji;

(e) kumtaka mtu yeyote katika chombo au jengo lolote kwa ajili ya kumsaida katika kuchunguza kontena lolote, mtego wa uvuvi, maliasili za uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji, hati au kitu chengine chochote katika chombo cha baharini, chombo cha moto au jengo jengine lolote kuhakikisha utekelezaji wa Sheria hii;

(f) kuandaa ripoti ya ukaguzi;

(g) kutoa maelekezo kwa mtuhumiwa kuleta chombo cha moto, ndege, chombo cha baharini katika kituo cha karibu ambapo kosa limefanyika; na

(h) kufuatilia lalamiko lolote lililowasilishwa kwa Mamlaka na kuchukua hatua.

Waangalizi wa uvuvi.

21.-(1) Mkurugenzi Mkuu atateua miongoni mwa maafisa waliyoidhinishwa wa Mamlaka kuwa waangalizi wa uvuvi.

(2) Muangalizi wa uvuvi aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) atakusanya, ataweka kumbukumbu na atatoa taarifa sahihi zinazohusiana na uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji kwa madhumuni ya uhifadhi, usimamizi na ufuatiliaji ikijumuisha:

(i) uvunaji, utunzaji na uchakataji wa samaki na bidhaa za samaki, mazao yatokanayo na ukuzaji wa viumbe maji na shughuli zinazohusiana; na

(ii) usafirishaji, uhaulishaji wa samaki baharini, uhifadhi au uteketezaji wa samaki au bidhaa za samaki au mazao yatokanayo na ukuzaji wa viumbe maji;

(b) atafuatilia utekelezaji wa hatua zilizochukuliwa za uhifadhi na usimamizi kwa mujibu wa Sheria hii; na

(c) atatekeleza wajibu mwengine wowote kama anavyoweza kupewa na Mkurugenzi Mkuu.

Uingizaji na usafirishaji nje ya nchi wa mitego ya uvuvi na vifaa.

22. Mtu ambaye anakusudia kuingiza au kusafirisha nje ya nchi mitego ya uvuvi au vifaa ataomba kibali kwa Mamlaka katika namna kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Katazo la mitego, vifaa na mbinu za uvuvi haribifu.

23.-(1) Mtu ambaye anakusudia kufanya shughuli yoyote ya uvuvi:

(a) hatotumia mtego wa uvuvi uliokatazwa, kifaa au njia yoyote haribifu;

(b) hatotumia nyavu ya kuvulia au dema lenye macho madogo na ya aina nyengine tofauti na ukubwa na aina inayoruhusiwa katika eneo husika;

(c) hatomiliki mtego au kifaa cha uvuvi kilichokatazwa katika maeneo ya maji ya ndani na maji ya Nchi;

(d) hatoburuza au hatokokota aina yoyote ya nyavu ya kuvulia katika maji ya ndani na maji ya Nchi;

(e) hatotumia mchanga au kitu chengine ambacho kinatumika kuisaidia nyavu ya uvuvi ambacho kinaweza kuathiri au kusababisha uharibifu wa mfumo wa ikolojia wa baharini;

(f) hatotumia miripuko, sumu au kemikali yoyote yenye kulewesha samaki; au

(g) hatobeba, hatomiliki au kuwa na milipuko, sumu au kemikali nyengine yoyote yenye kulewesha.

(2) Mtu yeyote ambaye atakutwa na umiliki wa samaki pamoja na mitego, vifaa na mbinu za uvuvi haribifu atachukuliwa kuwa anajihusisha na uvuvi usioruhusiwa.

(3) Mtu ambaye amekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

(4) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1)(c) cha kifungu hiki, endapo mtego au kifaa cha uvuvi kilichokatazwa kutumika katika eneo fulani kinasafirishwa, kitahifadhiwa katika namna kama itakavyoelezwa katika kanuni.

(5) Mripuko, sumu au kitu chengine chenye kulewesha kilichokutwa ndani ya chombo chochote cha uvuvi kitachukuliwa, isipokuwa ikithibitishwa vyenginevyo, kuwa kimetumika kwa madhumuni yaliyotajwa katika kifungu kidogo cha (1)(f) cha kifungu hiki.

(6) Endapo mtu amekutwa katika maji ya ndani au maji ya Nchi mara baada ya mripuko, sumu au kitu chenye kulewesha kutumika, mtu huyo atachukuliwa kuwa ametumia mripuko, sumu au kitu chenye kulewesha hicho mpaka itakapothibitishwa vyenginevyo.

(7) Mamlaka inaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kuweka orodha ya mitego, vifaa au njia za uvuvi zilizokatazwa.

Katazo la uvuvi, ushushaji na uuzaji wa samaki.

24. Mtu:

(a) hatovua, hatoshusha na hatomiliki samaki ambaye ameharibiwa au amethibitika kuharibiwa au amevuliwa katika eneo lililotangazwa kuwa limeharibika;

(b) hatovua, hatoshusha na hatomiliki samaki ambaye ni mchanga au wa chini ya kiwango cha ukubwa uliowekwa kwa aina hiyo ya samaki kama itavyoelezwa katika kanuni;

(c) hatouza, hatonunua, au hatopokea samaki kwa kujua au kuwa na sababu ya kuamini kwamba samaki huyo amevuliwa kinyume cha aya ya (a) au (b) ya kifungu hiki; au

(d) hatoshusha samaki katika bandari ya uvuvi au diko ambalo halijatangazwa.

Uwekaji wa vifaa vya kuvutia samaki au mwamba bandia.

25.-(1) Mtu anaweza, baada ya ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu, kuweka kifaa cha kuvutia samaki, mwamba bandia au kitu chengine chochote kinachofanana kwa madhumuni ya uvuvi katika maji ya ndani au maji ya Nchi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, masharti ya ruhusa yataelezwa katika kanuni.

(3) Ruhusa ya kuweka kifaa cha kuvutia samaki haitatoa haki ya kipekee kuvua samaki karibu na kifaa hicho, na hakuna mtu atakayedai haki hiyo.

Katazo la kuvuruga au kuharibu mtego wa uvuvi.

26.-(1) Mtu:

(a) hatotoa samaki yoyote katika mtego wa uvuvi isipokuwa mtu huyo ni mmiliki au atatoa kwa idhini ya mmiliki; au

(b) hatovuruga, hatoharibu, hatotoa, au hatochukua sehemu yoyote katika kifaa cha kuvutia samaki, mwamba bandia, boya, mtego, dema au kifaa chengine kilichoidhinishwa na kuwekwa kwa mujibu wa Sheria hii kinachomilikiwa na mtu mwengine.

(2) Mtu ambaye amekiuka masharti ya kifungu hiki ametenda kosa.

Ufuatiliaji.

27. Mamlaka itaweka utaratibu wa kuhakikisha ufuatiliaji wa samaki na bidhaa za ukuzaji wa viumbe maji.

Ushajishaji wa uvuvi mdogo na kusaidia uvuvi wa viwanda.

28.-(1) Mamlaka, kwa kushirikiana na taasisi zinazohusika, itasaidia uvuvi wa kibiashara na itashajiisha na italinda uvuvi mdogo endelevu.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu atatoa miongozo kwa ajili ya kushajiisha na kulinda uvuvi mdogo pamoja na kusaidia uvuvi wa viwanda kwa mujibu wa miongozo ya kimataifa au kikanda.

Kutangazwa kwa diko na bandari ya uvuvi.

29.-(1) Waziri, baada ya mapendekezo ya Mkurugenzi Mkuu na kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, atatangaza diko na bandari za uvuvi.

(2) Diko na bandari za uvuvi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, zitasimamiwa na zitaendeshwa katika namna itakavyoelezwa katika kanuni.

(3) Mtu ambaye anashusha samaki katika eneo lolote isipokuwa diko au bandari ya uvuvi iliyotangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

SEHEMU YA TANO
USAJILI WA WAVUVI NA UTOAJI LESENI WA VYOMBO VYA UVUVI

Usajili wa shughuli za uvuvi.

30.-(1) Mvuvi au mtu ambaye anakusudia kujihusisha katika shughuli zozote zinazohusiana na uvuvi ataomba usajili kwa Mamlaka kwa mujibu wa taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mamlaka itaweka aina za shughuli zinazohusiana na uvuvi.

(3) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Leseni na uvuvi.

31.-(1) Mtu au chombo cha uvuvi ambacho kinakusudia kujihusisha katika uvuvi kitaomba leseni kwa Mamlaka kwa mujibu wa taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

(2) Mamlaka inaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, itaanzisha aina za leseni na kuweka kiwango cha ada kwa kuzingatia aina, ukubwa na uwezo wa vyombo vya baharini, aina za samaki na vigezo vyengine vinavyohusika.

(3) Leseni zitakazotolewa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, zitatumika kwa:

(a) vyombo vya uvuvi wa kiviwanda au shughuli zinazohusiana;

(b) vyombo vya uvuvi wa kati au shughuli zinazohusiana;

(c) vyombo vya uvuvi mdogo wa kibiashara au shughuli zinazohusiana;

(d) vyombo vya uvuvi wa michezo au shughuli zinazohusiana;

(e) ukuzaji wa viumbe maji; na

(f) shughuli nyengine yoyote ndani ya mawanda ya Sheria hii.

Usimamishwaji na ufutaji wa leseni.

32.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kusimamisha au kufuta leseni endapo mmiliki wa leseni ameshindwa kufuata masharti ya Sheria hii au sharti lolote la leseni.

(2) Taratibu na sababu za usimamishaji au ufutaji wa leseni zitakuwa kama zilivyoelekezwa katika kanuni.

SEHEMU YA SITA
USIMAMIZI WA UKUZAJI WA VIUMBE MAJI

Usajili wa miundombinu na shughuli za ukuzaji wa viumbe maji.

33. Mtu ambaye anakusudia kuanzisha miundombinu au shughuli za ukuzaji wa viumbe maji ataomba usajili wa miundombinu au shughuli hiyo kwa Mamlaka kwa kuzingatia taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

Leseni ya uendeshaji wa shughuli za ukuzaji wa viumbe maji.

34.-(1) Mtu ambaye anakusudia kuendesha shughuli za ukuzaji wa viumbe maji ataomba leseni kwa Mamlaka kwa kuzingatia taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba:

(a) maendeleo ya ukuzaji wa viumbe maji ni endelevu na yanaruhusu matumizi yenye mantiki ya rasilimali zinazotumikia kwa pamoja kwa ukuzaji wa viumbe maji na shughuli nyengine; na

(b) mfumo wa maisha, utamaduni na mila za jamii pamoja na ufikaji wao katika maeneo ya uvuvi hautoathiriwa na shughuli za ukuzaji wa viumbe maji.

(3) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Uingizaji, uhamishaji na usafirishaji nje wa viumbe vya maji ya baharini na maji baridi na bidhaa zake.

35.-(1) Mtu, kwa kuzingatia ruhusa iliyotolewa na Mkurugenzi Mkuu:

(a) ataingiza, ataachia au atasababisha uingizaji au ataachia aina za mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi wa kigeni katika mifumo ya maji ya Zanzibar;

(b) atahamisha mayai, vifaranga au mbegu zozote za kigeni au viumbe waliopevuka wanaofanana kutoka moja ya miundominu ya ukuzaji wa

viumbe maji kwenda nyengine au kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine; au

(c) atasafirisha nje mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi, mayai au vifaranga kwa madhumuni ya ukuzaji wa viumbe wa maji.

(2) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

(3) Ruhusa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatolewa kwa kuzingatia taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

Vibali vya ukuzaji wa viumbe maji.

36.-(1) Mtu ambaye anakusudia kujenga miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji ataomba kibali cha ukuzaji wa viumbe maji kwa Mamlaka kwa mujibu wa taratibu zitakazoelezwa katika kanuni.

(2) Kibali cha ukuzaji wa viumbe maji kitampa mmiliki wa kibali haki ya kipekee ya kuvuna bidhaa za ukuzaji wa viumbe maji ndani ya eneo lililoainishwa katika kibali.

(3) Kibali cha ukuzaji wa viumbe maji hakitohaulishwa bila ya idhini ya maandishi ya Mkurugenzi Mkuu.

(4) Mtu yeyote ambaye anaekiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa.

Ujenzi, uendeshaji na uondoaji wa miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji.

37.-(1) Miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji itajengwa na kuendeshwa ndani ya maeneo yaliyoidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

(2) Mmiliki wa kibali hatotakiwa kufanya ujenzi wowote wa miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji ambao unazuia:

(a) usafiri huru wa maji unaopita au unaopakana na maeneo ya uzio wa samaki, vizimba, mitego au mabwawa;

(b) mtiririko wa maji ya mawimbi kwenda na kutoka eneo hilo; au

(c) shughuli nyengine yoyote katika eneo la baharini.

(3) Miundombinu ya ukuzaji wa viumbe maji yoyote inayokiuka masharti ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki itaondolewa kwa gharama za mmiliki wa kibali.

(4) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, mmiliki wa kibali kwa gharama zake mwenyewe atarudisha eneo lililoharibika ambalo lilitumika kwa ajili ya shughuli ya ukuzaji wa viumbe maji.

Udhibiti wa maradhi.

38.-(1) Mkurugenzi Mkuu, endapo bidhaa za ukuzaji wa viumbe maji katika eneo lolote zimeathiriwa na maradhi yoyote au zimesababisha athari kwa mazingira au shughuli nyengine za ukuzaji wa viumbe maji, atatoa taarifa kwa mmiliki wa kibali inayomtaka kuharibu bidhaa zote katika eneo husika au kuchukua hatua nyengine kama zitakavyoainishwa katika taarifa.

(2) Mmiliki wa kibali, baada ya kupokea taarifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atafuata masharti yaliyowekwa kwa gharama zake.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza kuchukua hatua yoyote muhimu ili kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya taarifa na gharama zilizotumika zimerejeshwa kutoka kwa mmiliki wa kibali.

Hatua za kuzuia.

39. Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti Rasmi, kuweka hatua za kuzuia kuhusiana na hifadhi ya samaki au eneo lililoathirika au vyote, kama Mkurugenzi Mkuu ataona ni muhimu na katika mazingira ambayo ameridhika kwamba, kuna:

(a) matukio ya ugonjwa;

(b) tishio kubwa la kupungua kwa wingi au kupoteza uwezo wa kuzaliana kwa samaki wa aina moja au zaidi; au

(c) mabadiliko makubwa ya mazingira ya majini.

SEHEMU YA SABA
USIMAMIZI NA VIWANGO VYA UBORA VYA SAMAKI NA BIDHAA ZA MAJINI

Mamlaka yenye uwezo.

40.-(1) Mamlaka itakuwa ni mamlaka yenye uwezo kwa ajili ya kuhakiki na kuthibitisha utekelezaji wa masharti ya uvuvi na bidhaa za majini.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mamlaka yenye uwezo:

(a) itatoa kibali kwa ajili ya uanzishwaji wa kiwanda cha uchakataji wa samaki, vyumba baridi, mitambo ya barafu, vyombo vya moto vya kusafirishia samaki, boti na diko;

(b) itatoa cheti cha afya kwa usafirishaji wa samaki na bidhaa za baharini nje ya nchi;

(c) itatoa cheti cha usafi kabla samaki na bidhaa za majini kuwekwa sokoni ili kuhakikisha ubora wao;

(d) itasajili waingizaji na wasafirishaji wa samaki, bidhaa za samaki na za majini;

(e) itaanzisha mfumo wa ufuatiliaji na uwekaji wa alama kwa samaki na bidhaa za majini;

(f) itafanya uangalizi wa viashiria hatarishi kupitia ukaguzi wa vyombo vya uvuvi, viwanda, sehemu ya kuhifadhia, mitambo ya barafu, diko, shehena na jengo jengine lolote kwenye mnyororo wa thamani wa sekta ya uvuvi na ukuzaji wa viumbe maji kabla ya kusafirisha nje ya nchi na kwa matumizi ya ndani ya nchi; na

(g) itatekeleza jukumu jengine lolote kama mamlaka yenye uwezo.

Uingizaji wa samaki hai.

41.-(1) Mtu hatoingiza samaki hai kwa ajili ya ukuzaji wa viumbe maji au kwa madhumuni ya mapambo bila ya ruhusa itakayotolewa na Mamlaka.

(2) Mamlaka haitotoa ruhusa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, isipokuwa:

(a) samaki huyo amewekwa chini ya uangalizi na udhibiti kwa kipindi maalum na kwa vigezo na masharti yatakayoelezwa katika kanuni;

(b) tathmini imefanywa kuhusiana na athari za mazingira ya kuachiliwa kwa samaki na muingizaji; na

(c) Mamlaka imeridhika, kupitia ripoti iliyowasilishwa na muingizaji, kuwa kuachiliwa kwa samaki hai huyo hakutoleta athari katika mazingira.

(3) Mamlaka inaweza kukataza uingizaji wa samaki hai yoyote ambaye anaweza kuleta athari katika mazingiza, ikijumuisha aina ya samaki aliyeainishwa kama vamizi, au ambaye anaweza kuleta hatari za kibaiolojia.

(4) Endapo Mkurugenzi Mkuu ana sababu za msingi za kushuku kwamba samaki hai yoyote ambaye ameingizwa Zanzibar hafai kwa ukuzaji wa viumbe maji au kwa madhumuni ya mapambo, ataamuru samaki huyo kuzuiliwa na kuharibiwa.

(5) Samaki hai yoyote aliyekatazwa kuingizwa **atazuiliwa na** ataharibiwa katika sehemu ya kuingia, au katika eneo la karantini au sehemu nyengine yoyote ambayo ipo kwa maonesho au kwa ajili ya mauzo.

(6) Bila ya kujali sheria nyengine yoyote, muingizaji wa samaki hai aliyeharibiwa chini ya kifungu hiki hatostahiki kupewa fidia yoyote.

(7) Mtu yeyote ambaye amekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

Taratibu za karantini kwa ajili ya uingizaji wa samaki hai wa mapambo.

42.-(1) Samaki hai wa mapambo yoyote aliyeingizwa Zanzibar atawekwa karantini kama itakavyoamuliwa na Mamlaka katika eneo la karantini lililoidhinishwa.

(2) Mamlaka itakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi wa baada wa karantini wa kituo cha kutotolea, kituo cha kulelea au shamba lolote la samaki.

(3) Endapo samaki hai wa mapambo aliyeingizwa Zanzibar hajapitia taratibu za karantini, samaki hai wa mapambo huyo, kwa gharama za muingizaji, atateketezwa kwa mujibu wa maelekezo yanayoweza kutolewa na Mamlaka.

(4) Bila ya kujali sheria nyengine yoyote, muingizaji wa samaki hai wa mapambo aliyeharibiwa chini ya kifungu hiki hatostahiki kulipwa fidia yoyote.

Katazo la kutupa au kuachia samaki hai wa mapambo aliyeingizwa.

43.-(1) Mtu hatotupa au hatoachia samaki hai wa mapambo aliyeingizwa katika sehemu yoyote ya maji.

(2) Mtu yeyote ambaye amekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

SEHEMU YA NANE
UHIFADHI NA USIMAMIZI WA BAHARI

Kutangazwa Maeneo ya uhifadhi wa bahari.

44.-(1) Waziri anaweza, kwa amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutangaza eneo lolote ndani ya mwambao, maji ya ndani au maji ya Nchi kuwa Eneo la Uhifadhi wa Bahari.

(2) Eneo lililotangazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki:

(a) liwe lina thamani ya mandhari ya asili, kisayansi, kihistoria, au thamani nyengine muhimu;

(b) liwe ni muhimu kulihifadhi, kuruhusu ufikiaji, au kuruhusu umma kuburudika na muonekano wa eneo hilo; au

(c) liwe limebainika kuwa na viumbe hai wa kipekee, maeneo ya kuzaliana au makaazi ya mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi.

(3) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza, kutangaza Eneo lolote la Uhifadhi wa Bahari au sehemu yoyote ya Eneo la Uhifadhi wa Bahari kuwa Eneo Maalumu, Eneo la Kurejesha Rasilimali za Uvuvi au Eneo lililotengwa kwa ajili ya matumizi maalumu.

(4) Eneo la Uhifadhi wa Bahari, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo katika tangazo la kutangaza eneo hilo au Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari eneo hilo, litajumuisha eneo lote la maji ya bahari na fukwe, ardhi ya pwani, maji, anga na tabaka za chini ya ardhi ndani ya mipaka ya eneo lililotangazwa.

(5) Maeneo yaliyotangazwa chini ya masharti ya kifungu hiki yatakuwa chini ya usimamizi na uangalizi wa Mamlaka.

Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari.

45.-(1) Mamlaka itatayarisha Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari ambao maudhui yake na utaratibu wa utayarishaji utaelezwa katika kanuni.

(2) Mamlaka, katika kutayarisha Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari, itashauriana na jamii na watu wengine ambao wanaweza kuathirika na mpango huo.

(3) Kila Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari uliotayarishwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki utawasilishwa katika Bodi kwa ajili ya kuidhinishwa.

(4) Shughuli yoyote ambayo haijajumuishwa katika Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari ndani ya Maeneo ya Uhifadhi wa Bahari itafanywa baada ya kuidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu.

Hatua za usimamizi wa uhifadhi.

46.-(1) Kutakuwa na hatua za usimamizi za Eneo la Bahari kama zitakavyoelezwa katika kanuni ili kuhakikisha uhifadhi endelevu wa Eneo la Bahari.

(2) Mkurugenzi Mkuu atatayarisha, atatekeleza, atafuatilia na atasimamia hatua za usimamizi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Ulinzi wa mifumo ya ikolojia ya bahari.

47.-(1) Mtu yeyote hatojihusisha katika shughuli yoyote ambayo inaharibu mifumo ya ikolojia ya bahari au aina yoyote ya mimea, hatoharibu, hatovunja au hatochukua

miamba ya matumbawe, mawe ya matumbawe, mafungu ya mchanga au mawe ya baharini kwa madhumuni yoyote.

(2) Mtu ambaye anakusudia kufanya shughuli za kawaida au kuweka miamba bandia, kifaa au kitu chengine chochote kwa madhumuni yoyote ndani ya Maeneo ya Uhifadhi wa Bahari atatakiwa kupata kibali kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, shughuli za kawaida zinajumisha kuchimba, kukata vinamasi, kufanya utafiti wa mitetemo na shughuli za ujenzi.

(4) Taratibu, vigezo na masharti ya utoaji wa kibali chini ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki zitaelezwa katika kanuni.

Uanzishwaji wa ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini kwenye kizuizi maalumu.

48.-(1) Mtu hatoanzisha ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini kwenye kizuizi maalumu bila ya kibali kutoka kwa Mamlaka.

(2) Mtu yeyote ambaye amekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

(3) Taratibu za kuanzisha ufugaji wa samaki na viumbe vya baharini kwenye kizuizi maalumu zitaelezwa katika kanuni.

Ulinzi wa viumbe vilivyo hatarini kutoweka au vilivyo-hifadhiwa.

49.-(1) Mtu, isipokuwa kwa ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu, hatovua, hatoshusha, hatouza, hatoshughulikia, hatosafirisha, hatopokea, hatonunua, hatomiliki, hatoingiza au hatosafirisha nje ya nchi viumbe vilivyo hatarini kutoweka au vilivyohifadhiwa kwa mujibu wa kifungu hiki.

(2) Endapo mtu amevua viumbe vilivyo hatarini kutoweka au vilivyohifadhiwa kwa bahati mbaya, mtu huyo:

(a) ikiwa kiumbe hicho kipo hai, atakiachia kiumbe hicho na kutoa taarifa kwa Mamlaka; na

(b) ikiwa kiumbe hicho kimekufa, atatoa taarifa kwa Mamlaka.

(3) Endapo mtu amekuta kiumbe kilicho hatarini kutoweka au kilichohifadhiwa kimekimbiwa na maji ikiwa kimekufa au kipo hai, atatoa taarifa kwa Mamlaka.

(4) Mtu yeyote ambaye amekiuka masharti ya kifungu hiki, ametenda kosa.

Utangazaji na uhifadhi wa viumbe adimu, waliyopo kwenye tishio au waliyo hatarini kutoweka.

50.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutangaza mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi kuwa viumbe adimu, waliyopo kwenye tishio au waliyo hatarini kutoweka.

(2) Mkurugenzi Mkuu ataweka hatua za uhifadhi endapo mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi wametangazwa kuwa viumbe adimu, waliyopo kwenye tishio au waliyo hatarini kutoweka chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza na kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kutoa tangazo endapo kiumbe chochote kilichotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kitasita kuwa adimu, kilichopo kwenye tishio au kilicho hatarini kutoweka.

(4) Mtu ambaye atakamata, atauza au atanunua kiumbe chochote chini ya kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano na isiyozidi Shilingi Milioni Thelathini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Katazo la kuwinda, kuua na kujeruhi mamalia wa baharini na viumbe vyote vya jamii ya kasa.

51.-(1) Mtu hatowinda, hatoua au hatojeruhi mamalia wa baharini na viumbe vyote vya jamii ya kasa.

(2) Mtu ambaye amekiuka masharti chini ya kifungu hiki, ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi na isiyozidi Shilingi Milioni Hamsini au kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Ulinzi wa eneo maalumu na eneo la kurejesha rasilimali za uvuvi.

52.-(1) Mtu, ndani ya eneo maalumu au eneo la kurejesha rasilimali za uvuvi:

(a) hatovua, hatowinda au hatokamata samaki au mnyama yoyote au kuondoa yai, viota au mbegu;

(b) hatokusanya, hatoondoa mimea au wanyama wa maji ya baharini na maji baridi, wakiwa hai au wamekufa, au mchanga, madini au mabaki ya majini;

(c) hatouza au hatosafirisha mimea au wanyama wa maji ya baharini na maji baridi, au bidhaa zake au mchanga, madini au mabaki ya majini;

(d) hatomiliki silaha yoyote, milipuko, dema au sumu;

(e) hatojihusisha na ukuzaji wa viumbe maji;

(f) hatofanya michezo ya uvuvi au shughuli nyengine yoyote ya kibiashara;

(g) hatosafisha au hatolima ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo chochote au uendeshaji wa mashine;

(h) hatojenga au hatoongeza jengo lolote, daraja au kazi nyengine yoyote; au

(i) hatoharibu, hatopaka au hatoondoa kitu chochote.

(2) Mtu yeyote ambaye amekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ametenda kosa.

(3) Mkurugenzi Mkuu anaweza kutoa muongozo kuruhusu shughuli zozote chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

Uchafuzi wa maeneo ya bahari.

53.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kutangaza eneo lolote la bahari kuwa limeharibiwa ikiwa eneo hilo limechafuliwa kwa vichafuzi au vitu vya sumu.

(2) Mtu yeyote hatochafua moja kwa moja au vyenginevyo eneo la bahari kwa namna yoyote ambayo inaweza kusababisha uharibifu au kushusha ubora wa eneo la bahari au mfumo wa ikolojia wa baharini.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, uchafuzi wa eneo la bahari unajumuisha:

(a) kutupa takataka au mabaki yasiyooza;

(b) kutupa kemikali zenye sumu au kitu cha hatari, ikijumuisha mafuta, petroli, vimumunyisho, vyuma au maji machafu; au

(c) kufanya kitendo chochote ambacho kinaweza kusababisha uharibifu au kushusha ubora wa eneo la bahari na mfumo wa ikolojia ya baharini.

Masharti ya kibali katika Eneo la Bahari.

54.-(1) Mtu ambaye anakusudia kufanya shughuli yoyote au kuingiza chombo chochote cha bahari katika Eneo la Bahari ataomba kibali kwa Mamlaka kwa mujibu wa taratibu zilizoelezwa katika kanuni.

(2) Mkurugenzi Mkuu anaweza, kwa amri itakayochapishwa katika Gazeti Rasmi, kuanzisha aina za vibali kwa ajili ya kufanya shughuli yoyote katika maeneo ya bahari.

(3) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, mtu ambaye anakusudia kuingia katika eneo la uhifadhi wa bahari, atalipa ada ya kiingilio kama itakavyoainishwa katika kanuni.

Mkakati wa ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi.

55.-(1) Mkurugenzi Mkuu ataandaa na atatekeleza Mkakati wa ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi katika maji ya ndani na maji ya Nchi.

(2) Mamlaka, kwa kushirikiana na mamlaka husika, itafanya ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi ndani ya maji ya ndani na maji ya Nchi.

SEHEMU YA TISA
MASHARTI YA FEDHA

Fedha na rasilimali za Mamlaka.

56.-(1) Fedha na rasilimali za Mamlaka zitajumuisha:

(a) fedha zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) fedha zinazopokelewa na Mamlaka kwa huduma zinazotolewa na Mamlaka;

(c) ruzuku halali, zawadi, michango, misaada au mikopo kama Mamlaka itakavyopokea kutoka kwa mtu au taasisi yoyote;

(d) ada na tozo zinazokusanywa chini ya Sheria hii; na

(e) fedha nyengine zozote zinazoweza kupatikana kihalali na Mamlaka.

(2) Mamlaka itabakiza asilimia maalumu ya fedha zilizokusanywa kama itakavyoamuliwa na Waziri anayehusika na fedha.

(3) Miamala yote ya kifedha ya Mamlaka itafanywa na kusimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

Bajeti ya Mamlaka.

57.-(1) Mkurugenzi Mkuu, katika kila mwaka wa fedha, ataanda na atawasilisha katika Bodi kwa ajili ya majadiliano na mapendekezo ya makadirio ya kina ya mapato na matumizi ya Mamlaka kwa mwaka wa fedha unaofuata.

(2) Baada ya majadiliano na mapendekezo ya Bodi, bajeti ya Mamlaka itachukuliwa kuwa sehemu ya bajeti ya Wizara.

(3) Makadirio ya mapato na matumizi ya Mamlaka yataandaliwa kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya 2016.

(4) Mkurugenzi Mkuu atahakikisha kwamba, malipo yote yanayofanywa kutokana na fedha za Mamlaka yanafanywa kwa usahihi na yanaidhinishwa ipasavyo na udhibiti wa kutosha unadumishwa juu ya mali na madeni ya Mamlaka.

Hesabu na ukaguzi.

58.-(1) Mamlaka itaweka hesabu na kumbukumbu za miamala yake na itahakikisha kwamba, fedha zote zilizopokelewa na kulipwa na Mamlaka zinasimamiwa vizuri.

(2) Taarifa za fedha za mwaka za Mamlaka zitakaguliwa kwa mujibu wa masharti ya sheria za fedha na sheria nyengine yoyote husika.

Ufunguaji wa hesabu za benki.

59. Mamlaka, kwa mujibu wa masharti ya sheria za fedha, itafungua hesabu ya benki kwa ajili ya utekelezaji mzuri ya kazi zake chini ya Sheria hii.

SEHEMU YA KUMI
MAKOSA NA ADHABU

Makosa na Adhabu.

60. Mtu ambaye:

(a) amejihusisha na shughuli za uvuvi au ufugaji wa viumbe maji bila ya kuwa na leseni au kibali;

(b) ameingiza au amesafirisha nje ya nchi mimea na wanyama wa maji ya baharini na maji baridi na bidhaa zao kinyume na masharti ya Sheria hii;

(c) ameharibu Eneo lolote la Uhifadhi wa Bahari;

(d) amejihusisha katika shughuli yoyote ambayo inaharibu mifumo ya ikolojia ya bahari;

(e) ametumia, amemiliki au amekuwa nayo katika chombo cha uvuvi, mitego ya samaki iliyokatazwa;

(f) ameweka kifaa cha kuvutia samaki, mwamba bandia au kitu chengine chochote kinachofanana kwa madhumuni ya uvuvi katika maji ya ndani au maji ya Nchi bila ya ruhusa ya Mkurugenzi Mkuu;

(g) amemzuia afisa yoyote aliyeidhinishwa katika kutekeleza kazi yoyote aliyopewa chini Sheria hii;

(h) amemzuia, amemuingilia, amemuwekea kikwazo au amemsumbua mvuvi aliyesajiliwa katika kufanya shughuli zake za uvuvi;

(i) amezuia ufikaji wa jamii yoyote katika maeneo ya bahari bila ya sababu za msingi;

(j) amevua, ameshusha au amemiliki samaki kwenye eneo ambalo limetangazwa kuwa eneo ambalo limeharibiwa au samaki wadogo wa chini ya kiwango cha ukubwa uliowekwa kwa aina hiyo ya samaki;

(k) ameshusha samaki yoyote katika bandari ya uvuvi au diko ambalo halijatangazwa; au

(l) amejihusisha na shughuli za uvuvi au ukuzaji wa viumbe maji bila ya usajili.

ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tatu za Kitanzania na isiyozidi Shilingi Milioni Kumi na Tano za Kitanzania au kifungo cha kipindi kisichopungua miezi sita, au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Adhabu ya ziada.

61. Mtu yeyote atakapotiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria hii, Mahakama inaweza, mbali na adhabu aliyopewa chini ya Sheria hii, kuamuru:

(a) endapo miundombinu yoyote au ikolojia imeharibiwa, imeathiriwa au imeondolewa kwa dhamira ya kufanya kosa, mtu huyo atalipa fidia inayofanana na thamani ya miundombinu au ikolojia iliyoharibiwa; au

(b) mali iliyotumika katika kutenda kosa kutaifishwa au kuharibiwa.

Adhabu ya Jumla.

62. Mtu yeyote ambaye amekwenda kinyume na masharti yoyote ya Sheria hii, ambapo hakuna adhabu maalumu iliyowekwa kwa kosa hilo, ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili na isiyozidi Shilingi Milioni Tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu, au adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Kumaliza kosa.

63.-(1) Mkurugenzi Mkuu anaweza kumaliza kosa lililofanywa na mtu chini ya Sheria hii au kanuni zake kwa kumtaka kulipa faini isiyopungua nusu ya faini iliyoainishwa kwa kosa hilo, endapo mtu:

(a) amekubali kwamba ametenda kosa; na

(b) atalipa malipo yote ya msingi chini ya Sheria hii.

(2) Taratibu zinazohusiana na kumaliza kosa zitaainishwa katika kanuni.

(3) Kumaliza kosa chini ya kifungu cha (1) cha kifungu hiki, hautochukuliwa kama ni hatia kwa kosa linaloshukiwa kufanywa na isipokuwa kwamba malipo ya msingi yamelipwa yote, hakutokuwa na mashtaka kwa kosa linaloshughulikiwa ambalo litafunguliwa au kuendelezwa.

SEHEMU YA KUMI NA MOJA
MASHARTI MENGINEYO

Uanzishwaji wa Kamati za Usimamizi wa pamoja.

64.-(1) Mamlaka itaanzisha Kamati za Usimamizi wa Pamoja za Uvuvi na Uhifadhi wa Bahari ambazo zitajumuisha wajumbe kutoka jamii ya eneo husika.

(2) Wigo, muundo, kazi na mambo mengine yanayohusiana na kamati zilizoanzishwa chini ya kifungu hiki yataelezwa katika kanuni.

Daftari la kumbukumbu.

65. Mkurugenzi Mkuu ataanzisha na kutunza daftari la kumbukumbu kwa ajili ya wavuvi, shughuli za ukuzaji wa viumbe maji, leseni na kibali kinachotolewa chini ya Sheria hii.

Vitu vyenye asili ya kuharibika.

66. Samaki au maliasili yoyote ya bahari yenye asili ya kuharibika itakayokamatwa chini ya Sheria hii inaweza, kwa maelekezo ya Mkurugenzi Mkuu, kushughulikiwa kwa mujibu wa Sheria husika.

Rufaa.

67.-(1) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi ya Mkurugenzi Mkuu anaweza kukata rufaa kwa Bodi ndani ya siku kumi na nne.

(2) Bodi, baada ya kupokea rufaa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itaamua rufaa hiyo ndani ya miezi mitatu.

(3) Mtu yeyote ambaye hajaridhika na uamuzi wa Bodi anaweza kukata rufaa kwa Waziri ndani ya siku kumi na nne.

(4) Waziri, baada ya kupokea rufaa, ataamua rufaa hiyo ndani ya siku ishirini na moja.

Kanuni.

68.-(1) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya ujumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga kanuni zinazohusiana na:

(a) taratibu za usimamizi wa pamoja;

(b) taratibu za maombi na utoaji wa leseni na vibali;

(c) katazo na usimamizi wa matumizi ya mitego na aina za uvuvi;

(d) hatua za usimamizi kwa uhifadhi endelevu wa Maeneo ya Bahari;

(e) maudhui na hatua za matayarisho ya Mpango Mkuu wa Usimamizi wa Bahari wa kila Eneo la Uhifadhi wa Bahari;

(f) masharti ya uingizaji au usafirishaji wa samaki na mazao ya baharini;

(g) orodha ya mitego na njia za uvuvi zilizokatazwa na zinazoharibu;

(h) vigezo vya uanzishwaji wa Maeneo Maalumu ndani ya Eneo la Uhifadhi wa Bahari;

(i) katazo au zuio la kuchukua, kukusanya, kuweka pamoja, kuua au kudhuru samaki wadogo na kuwaharibu samaki;

(j) masharti ya ruhusa na haki za matumizi ya vivutia samaki;

(k) kutangazwa bandari za uvuvi na madiko;

(l) vigezo vya uainishaji wa viwanda vya uchakataji wa samaki, vyumba vya baridi, mitambo ya barafu, vyombo vya kusafirishia samaki, boti na madiko;

(m) masharti chini ya waingizaji au wasafirishaji wa samaki na mazao ya baharini; na

(n) aina za leseni na kuweka madaraja tofauti ya tozo kwa kuzingatia aina, ukubwa na njia ya uendeshaji wa chombo, aina ya samaki na mambo mengine ya msingi.

Kufuta na kubakiza.

69.-(1) Sheria ya Uvuvi, Nam. 7 ya 2010 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, jambo lolote lililofanywa au limekusudiwa kufanywa chini ya Sheria iliyofutwa, litaendelea na kuchukuliwa kuwa limefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

JADWELI

MWENENDO WA BODI
[Chini ya kifungu cha 12]

Makamu Mwenyekiti.

1. Wajumbe wa Bodi watamchagua mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Muda wa wajumbe.

2. Isipokuwa wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watashika nafasi zao kwa kipindi cha miaka mitatu kutoka tarehe ya uteuzi wao na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine kimoja tu.

Vikao vya Bodi.

3.-(1) Bodi itakutana kikawaida kila baada ya miezi mitatu na inaweza kukutana muda wowote itakapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi zake.

(2) Vikao vyote vya Bodi vitaendeshwa na Mwenyekiti na ikiwa hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao cha Bodi na endapo Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti hawapo, wajumbe watakaokuwepo watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

Akidi.

4. Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe wote wa Bodi wataunda akidi katika kikao chochote cha Bodi.

Uamuzi ya Bodi.

5. Uamuzi ya Bodi utafanywa kwa maafikiano, endapo hakuna maafikiano, maamuzi yatafanywa kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti atakuwa na kura ya uamuzi.

Taratibu za Vikao.

6. Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kujipangia taratibu zake wenyewe kuhusiana na vikao na uendeshaji mzuri wa shughuli zake.

Mjumbe mualikwa.

7. Bodi inaweza kumualika mtu yeyote ambaye sio mjumbe wa Bodi kuhudhuria katika majadiliano yoyote ya kikao cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Kamati za Bodi.

8. Bodi inaweza, kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha kamati kwa ajili ya kutekeleza kazi maalumu kama itakavyoona inafaa.

Kumbukumbu za vikao vya Bodi.

9. Kumbukumbu za vikao vya Bodi zitathibitishwa na Bodi katika kikao kinachofuata na kutiwa saini na Mwenyekiti na Katibu.

Kukasimu kazi za Bodi.

10.-(1) Bodi inaweza, itakavyoona inafaa kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa Kamati za Bodi.

(2) Endapo Bodi itakasimu kazi zake chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatoa miongozo kwa maandishi endapo itahitajika ili kuhakikisha utekelezaji bora wa kazi.

Kubainisha maslahi.

11.-(1) Mjumbe wa Bodi ambaye ana maslahi ya moja kwa moja au vyenginevyo juu ya jambo linalohusika au linalotakiwa kuzingatiwa na Bodi, haraka iwezekanavyo baada kutambua, atabainisha uhalisia wa maslahi yake mwanzoni mwa kikao cha Bodi.

(2) Ubainishaji wa maslahi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, utawekwa katika kumbukumbu za kikao na mjumbe aliyebainisha:

(a) hatohudhuria katika majadiliano ya Bodi katika kufanya uamuzi; na

(b) hatamshawishi mjumbe mwengine yeyote katika kufanya uamuzi.

Kusita kuwa mjumbe.

12. Mjumbe atasita kushika nafasi yake ikitokea moja kati ya yafuatayo:

(a) amejiuzulu;

(b) ikiwa hatohudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi bila ya sababu za msingi;

(c) ikiwa atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya afya ya kimwili au kiakili;

(d) ikiwa atasita kuwa mwakilishi wa taasisi iliyomteua mjumbe huyo;

(e) ikiwa atasimamishwa na Waziri akishindwa kutimiza matarajio ya Mamlaka; au

(f) amefariki.

Posho la wajumbe wa Bodi.

13. Mwenyekiti na wajumbe wengine wa Bodi watasitahiki kulipwa posho kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011.

UMEPITISHWA na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 15 Septemba, 2026.

.....

(HASSAN ALI HAJI)

Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.